**SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUFUTA BAADHI YA KODI NA TOZO NA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI ZINAZOHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA SERIKALI**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.

**SEHEMU YA PILI**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI NA TARATIBU ZA KODI, NAM. 7 YA 2009**

2. Kusomwa.
3. Marekebisho ya kifungu cha 3.
4. Marekebisho ya kifungu cha 5.
5. Marekebisho ya kifungu cha 18.
6. Marekebisho ya kifungu cha 21.
7. Kuongeza kifungu kipya cha 21A.
8. Kuongeza kifungu kipya cha 21B.
9. Kuongeza kifungu kipya cha 21C.
10. Marekebisho ya kifungu cha 26.
11. Marekebisho ya kifungu cha 31.
12. Kuongeza kifungu kipya cha 49A.
13. Marekebisho ya kifungu cha 61.

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA RUFAA ZA KODI ZANZIBAR, NAM. 1 YA 2006

14. Kusomwa.

15. Marekebisho ya kifungu cha 3.

16. Kufuta vifungu vya 16,17,18 na 19.

17. Marekebisho ya kifungu cha 20.

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI, NAM. 4 YA 1998

18. Kusomwa.

19. Marekebisho ya kifungu cha 8.

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA MAJENGO NAM. 14 YA 2008

20. Kusomwa.

21. Kuongeza kifungu kipya cha 7A.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA HOTELI NAM. 1 YA 1995

22. Kusomwa.

23. Marekebisho ya kifungu cha 3.

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA NAM. 12 YA 2016

24. Kusomwa.

25. Marekebisho ya kifungu cha 29.

26. Marekebisho ya kifungu cha 30.

27. Marekebisho ya kifungu cha 80.

28. Marekebisho ya kifungu cha 111.

29. Marekebisho ya kifungu cha 119.

30. Marekebisho ya kifungu cha 121.

31. Kuongeza vifungu vipya vya 133A na 133B.

**SEHEMU YA NANE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA AJIRA NAM. 11 YA 2005**

32. Kusomwa.

33. Kuongeza kifungu kipya cha 38A.

34. Kufuta na kubakiza kifungu cha 39.

**SEHEMU YA TISA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA UKUZAJI NA KULINDA VITEGA UCHUMI ZANZIBAR NAM. 14 YA 2018**

35. Kusomwa.

36. Kuongeza kifungu kipya cha 31A.

**SEHEMU YA KUMI**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA NAM. 11 YA 2016**

37. Kusomwa .

38. Kuongeza kifungu kipya cha 73A.

**SHERIA NAM. 12 YA 2020**

**NIMESAINI**

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

29th June, 2020

# SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUFUTA BAADHI YA KODI NA TOZO NA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI ZINAZOHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA SERIKALI

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma), 2020 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI NA TARATIBU ZA KODI, NAM. 7 YA 2009

Kusomwa.

**2.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi na Taratibu za Kodi Nam. 7 ya 2009, katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**3.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 3, kwa kuingiza tafsiri ya maneno mapya "maamuzi ya pingamizi' katika mpangilio wa herufi kama ifuatavyo:

"maamuzi ya pingamizi" maana yake ni maamuzi ya mwisho yanayotolewa na Kamishna katika kuamua pingamizi kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**4.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 5, kwa kuongeza kifungu kidogo cha (7) kama ifuatavyo:

"(7) kwa madhumuni ya usimamizi mzuri wa kodi, Waziri anaweza kutunga kanuni za kuainisha majengo ya biashara kuhusiana na walipakodi".

Marekebisho ya kifungu cha 18.

**5.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 18:

(a) kwa kuongeza kifungu kidogo cha (4) mara baada ya kifungu kidogo cha (3) kama ifuatavyo:

"(4) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (2), Waziri anaweza, kwa amri iliyotangazwa katika Gazeti Rasmi, kuongeza muda wa mwisho wa kuwasilisha ritani ya kodi ama kwa ujumla au kisekta au kundi la walipa kodi kwa tarehe nyengine ambayo atakayoiamua endapo atazingatia kwamba kuna sababu ya msingi ya kuongeza huko na baada ya kupata idhini ya Baraza la Mapinduzi".

(b) kwa kukipa nambari mpya kifungu kidogo cha (4) kuwa kifungu kidogo cha (5) na kifungu kidogo cha (5) kuwa kifungu kidogo cha (6).

Marekebisho ya kifungu cha 21.

**6.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 21, kwa kufuta maneno "Sheria ya Rufaa za Kodi Zanzibar, Nam. 1 ya 2006" na kuweka badala yake maneno "masharti ya Sheria hii".

Kuongeza kifungu kipya cha 21A.

**7.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 21A mara baada ya kifungu cha 21 kama ifuatavyo:

"Pingamizi."

**21A.** (1) Mtu ambaye hajaridhika na maamuzi yaliyotolewa na Kamishna ikijumuisha makadirio ya kodi katika kutekeleza mamlaka yake chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote ya kodi, anaweza kupinga maamuzi kwa kuwasilisha pingamizi kwa Kamishna ndani ya siku thelathini kutoka tarehe aliyowasilishiwa maamuzi hayo.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtu yeyote hatotoa pingamizi kwa Kamishna dhidi ya yafuatayo:

(a) maamuzi ya kumkagua, kumpeleleza au kumkadiria mlipa kodi;

(b) hati ya utekelezaji au maamuzi au kutoamua kutoa, kukataa au kufuta hati ya utekelezaji;

(c) maamuzi au kutokutoa maamuzi ambayo yanamuathiri mtu kama ofisa wa kodi au muajiriwa au wakala wa kodi wa Bodi; na

(d) kumaliza kosa kwa ridhaa ya muombaji".

(3) Kwa kuzingatia masharti yaliyoelezwa katika kifungu hiki, Kamishna anaweza:

(a) kupokea notisi ya pingamizi; au

(b) kukataa kupokea notisi ya pingamizi.

(4) Mtu ambaye hajaridhika kwa kukataa Kamishna kupokea notisi ya pingamizi iliyotolewa, anaweza kukata rufaa kwa Bodi ya Rufaa za Kodi Zanzibar dhidi ya kukataa huko.

(5) Mtu ambaye atakuwa na sababu za msingi zinazopelekea kuongezwa muda wa kuwasilisha pingamizi dhidi ya maamuzi yaliyotolewa na Kamishna, anaweza kuomba kuongezewa muda kwa Kamishna.

(6) Endapo Kamishna ataridhika na sababu zilizoelezwa katika maombi yaliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki, atatoa muda wa ziada usiozidi siku thelathini na atatoa notisi ya maamuzi yake kuhusiana na kuongeza huko.

(7) Pingamzi dhidi ya maamuzi yoyote itakuwa katika utaratibu ulioelezwa katika Kanuni na itaeleza sababu ambazo pingamizi hiyo imetolewa.

(8) Pingamizi dhidi ya maamuzi yoyote haitopokelewa isipokuwa mlipakodi awe, siku au kabla ya siku ya mwisho ya kuwasilisha pingamizi, amelipa kiwango cha kodi ambacho hakipo katika mgogoro au theluthi moja ya kodi iliyokadiriwa kiwango chochote kitakachokuwa kikubwa, isipokuwa kwamba kodi yote au ushuru uliokadiriwa kuhusiana na uingizaji utachukuliwa kuwa haupo katika mgogoro.

(9) Endapo mtu amewasilisha notisi ya pingamizi bila kulipa kodi iliyoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (8), Kamishna hatoipokea notisi ya pingamizi na notisi ya pingamizi itachukuliwa kuwa haikuwasilishwa, isipokuwa kwamba, kifungu hiki kidogo hakitatumika kwa pingamizi ambayo haihusiani na ukadiriaji.

(10) Endapo Kamishna ataridhika kwamba kuna sababu za msingi zinazopelekea kupunguza au kusamehe, anaweza kupunguza au kusamehe kiwango kitakacholipwa chini ya kifungu kidogo cha (8).

(11) Endapo mlipakodi atawasilisha pingamizi na atafanya malipo chini ya kifungu kidogo cha (8), malipo yaliyobakia ya kodi iliyokadiriwa yataakhirishwa hadi pangamizi itakapoamuliwa.

Kuongeza kifungu kipya cha 21B.

**8.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 21B mara baada ya kifungu cha 21A kama ifuatavyo:

"Maamuzi ya pingamizi".

**21B.** (1) Kamishna, baada ya kupokea pingamizi kwa mujibu wa kifungu cha 21A, atatoa maamuzi kwa kuiamua pingamizi.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Kamishna anaweza kutaka ushahidi wowote au taarifa nyengine yoyote ikiwa ni muhimu katika kuiamua pingamizi na anaweza, kuhusiana na pingamizi dhidi ya makadirio:

(a) kurekebisha makadirio kwa mujibu wa pingamizi;

(b) kurekebisha makadirio kulingana na pingamizi na ushahidi wowote wa ziada ambao umewasilishwa; au

(c) kukataa kurekebisha makadirio.

(3) Endapo Kamishna:

(a) anakubali kurekebisha makadirio kwa mujibu wa pingamizi; au

(b) anapendekeza kurekebisha makadirio kulingana na pingamizi na ushahidi wowote wa ziada au taarifa iliyowasilishwa, na mtu aliyewasilisha pingamizi anakubaliana na Kamishna kwa marekebisho yaliyopendekezwa,

makadirio yatarekebishwa ipasavyo na Kamishna atawezesha notisi iliyoweka marekebisho hayo na kiwango cha kodi kinachopaswa kulipwa kuwasilishwa kwa mtu huyo.

(4) Endapo notisi ya pingamizi iliyotolewa na Kamishna hakuiamulia pingamizi hiyo ndani ya siku tisini, Kamishna atachukuliwa kuwa amekubali kurekebisha makadirio kwa mujibu wa pingamizi.

(5) Endapo Kamishna:

(a) anapendekeza marekebisho ya makadirio kulingana na pingamizi na ushahidi wowote wa ziada ambao uliwasilishwa, na mtu aliyewasilisha pingamizi hakubaliani na Kamishna kwa marekebisho yaliyopendekezwa, makadirio yatarekebishwa kama ilivyopendekezwa na Kamishna atawezesha notisi iliyoweka marekebisho hayo na kiwango cha kodi kinachopaswa kulipwa kuwasilishwa kwa mtu huyo; au

(b) anakataa kurekebisha makadirio, atawezesha notisi inayothibitisha makadirio kuwasilishwa kwa mtu huyo.

Kuongeza kifungu kipya cha 21C.

**9.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 21C mara baada ya kifungu cha 21B kama ifuatavyo:

"Kukamilika kwa makadirio".

**21C.** (1) Endapo, kuhusiana na makadirio yoyote:

(a) hakuna notisi ya pingamizi iliyotolewa; au

(b) notisi ya pingamizi imetolewa na:

(i) makadirio yamerekebishwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 21B cha Sheria hii; au

(ii) notisi imewasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu cha 21B cha Sheria hii lakini hakuna rufaa iliyowasilishwa; au

(iii) makadirio yameamuliwa kikamilifu katika rufaa,

makadirio kama yalivyofanywa au kama yalivyorekebishwa au yalivyoamuliwa katika rufaa, kama itakavyokuwa, yatakuwa ni ya mwisho na yamekamilika.

(2) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitamzuia Kamishna kufanya makadirio yoyote, ambayo hayatahusisha kufungua tena jambo lolote ambalo limeshaamuliwa katika rufaa au makadirio.

(3) Iwapo udanganyifu wowote au upuuzaji wowote uliofanywa na au kwa niaba ya mtu yeyote uliohusisha au unaohusu kodi yoyote, ushuru au tozo na unaathiri deni lake la kodi, Kamishna anaweza kufanya makadirio ya ziada kwa mtu huyo bila ya kujali kwamba itahusisha kufungua upya jambo ambalo limeamuliwa katika rufaa.

Marekebisho ya kifungu cha 26.

**10.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 26 kifungu kidogo cha (1) kwa:

(a) kuingiza neno "kupeleleza" baina ya maneno "kukagua" na "kuchunguza" yanayoonekana katika aya ya (a);

(b) kuingiza neno "upelelezi" baina ya maneno "ukaguzi" na "uchunguzi" yanayoonekana katika aya (b).

Marekebisho ya kifungu cha 31.

**11.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 31, kwa kuingiza kifungu kipya kidogo cha (5) mara baada ya kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo:

"(5) Bila ya kujali masharti ya kifungu hiki, Waziri anaweza, kwa amri iliyotangazwa katika Gazeti Rasmi, kuongeza muda wa mwisho wa kuwasilisha malipo ya kodi ama kwa ujumla au kisekta au kundi la walipa kodi kwa tarehe nyengine ambayo atakayoiamua endapo atazingatia kwamba kuna sababu ya msingi ya kuongeza huko na baada ya kupata idhini ya Baraza la Mapinduzi".

Kuongeza kifungu kipya cha 49A.

**12.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 49A mara baada ya kifungu cha 49 kama ifuatavyo:

"Kulinda taarifa binafsi".

49A. Bila ya kuathiri masharti ya vifungu 48 na 49 vya Sheria hii, ubadilishanaji na ukusanyaji wa taarifa za kodi utakuwa kwa mujibu wa viwango vya kulinda taarifa binafsi.

Marekebisho ya kifungu cha 61.

**13.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 61 kwa kufuta neno "yoyote" linaloonekana baina ya maneno "kwa" na "maamuzi" na kuweka badala yake maneno "pingamizi".

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA RUFAA ZA KODI ZANZIBAR, NAM. 1 YA 2006

Kusomwa.

**14.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Rufaa za Kodi Zanzibar Nam. 1 ya 2006, katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**15.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 3 kwa kuingiza tafsiri mpya ya maneno "maamuzi ya pingamizi" kwa mpangilio wa herufi kama ifuatavyo:

"maamuzi ya pingamizi" maana yake ni maamuzi ya mwisho yanayotolewa na Kamishna katika kuamua pingamizi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi na Taratibu za Kodi.

Kufuta vifungu vya 16,17,18 na 19.

**16.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta vifungu vya 16, 17, 18 na 19 vya Sheria.

Marekebisho ya kifungu cha 20.

**17.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 20 kwa:

(a) kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"20(1). Mtu ambaye hakuridhika na maamuzi ya pingamizi yaliyotolewa na Kamishna au kukataa Kamishna kupokea notisi ya pingamizi, anaweza kukata rufaa kwa Bodi dhidi ya maamuzi hayo ya pingamizi au kukataa huko, isipokuwa kwamba mtu huyo hatokata rufaa dhidi ya maamuzi ya pingamizi yanayohusiana na makadirio endapo Kamishna anaamua kurekebisha makadirio kwa mujibu wa pingamizi".

(b) kuingiza kifungu kidogo cha (2) mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, rufaa dhidi ya kukataa Kamishna kupokea notisi ya pingamizi inayohusiana na makadirio haitasikilizwa isipokuwa mlipa kodi awe amelipa kiwango cha kodi ambacho hakina mgogoro au theluthi moja ya makadirio ya kodi, kiwango chochote kitakachokuwa kikubwa.

(c) kukipa nambari mpya kifungu kidogo cha (2) kuwa kifungu kidogo cha (3) na kukiandika upya kama ifuatavyo:

(3) Bodi haitasikiliza rufaa kwa mujibu wa kifungu hiki isipokuwa:

(a) mkata rufaa awali aliwasilisha notisi ya rufaa ya maandishi kwa Kamishna na Bodi ndani ya siku kumi na nne kutoka tarehe aliyopewa maamuzi ya pingamizi; na

(b) rufaa iwe imewasilishwa katika Bodi ndani ya siku thelathini kutoka tarehe ambayo mkata rufaa alipewa maamuzi ya pingamizi.

(d) kukipa nambari mpya kifungu kidogo cha (3) kuwa kifungu kidogo cha (4) na kifungu kidogo cha (4) kuwa kifungu kidogo cha (5).

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI, NAM. 4 YA 1998

Kusomwa.

**18.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Nam. 4 ya 1998, katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 8.

**19.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 8 kwa kufuta neno "kumi na nane" linaloonekana baina ya maneno "ya" na "asilimia" na kuweka badala yake neno "kumi na tano".

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA MAJENGO NAM. 14 YA 2008

Kusomwa.

**20.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kodi ya Majengo Nam. 14 ya 2008, katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kuongeza kifungu kipya cha 7A.

**21.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 7A mara baada ya kifungu cha 7 kama ifuatavyo:

Waziri kuainisha jengo au aina za majengo.

"7A. (1) Bila ya kujali masharti ya vifungu vya 6 na 7 vya Sheria hii, Waziri anaweza, baada ya kupata idhini ya Baraza la Mapinduzi na kwa amri iliyotangazwa katika Gazeti Rasmi, kuainisha majengo au aina za majengo ambayo yanapaswa kulipiwa kiwango maalumu cha kodi ya majengo na kiwango maalumu cha kulipwa".

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Kamishna atakusanya kiwango maalumu cha kodi ya majengo kama ilivyoamuliwa na Waziri".

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA HOTELI NAM. 1 YA 1995

Kusomwa.

**22.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ushuru wa Hoteli Nam. 1 ya 1995, katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**23.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 3 kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"3(1) Kwa kuzingatia Sheria hii, kutatozwa na kukusanywa ushuru utakaojulikana kama ushuru wa hoteli kwa mwendeshaji wa hoteli, mkahawa na huduma nyengine za kitalii kwa kiwango cha asilimia kumi na mbili kwa thamani ya kodi ya huduma zinazotozwa".

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA NAM. 12 YA 2016

Kusomwa.

**24.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya 2016, katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 29.

**25.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 29 kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (4) mara baada ya kifungu kidogo cha (3) kama ifuatavyo:

"29(4) Bila ya kujali masharti ya kifungu hiki, Afisa Mas-uli atawajibika na usimamizi mzuri wa mikataba yote inayoingiwa na Taasisi yake ya Umma kama itakavyoainishwa katika Kanuni".

Marekebisho ya kifungu cha 30.

**26.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 30, kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (5) na cha (6) mara baada ya kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo:

"(5) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Afisa Mas-uli atawajibika kuhakikisha kwamba risiti zinatolewa kwa mapato yote yanayokusanywa na kwamba mapato yanapokewa, yanahifadhiwa na yanahesabiwa kwa ujumla wake.

(6) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, matumizi yoyote dhidi ya mapato yatahitaji idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali kama matumizi yaliyoingiwa na Serikali".

Marekebisho ya kifungu cha 80.

**27.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 80, kwa kuongeza vifungu vidogo vipya vya (6) na (7) mara baada ya kifungu kidogo cha (5) kama ifuatavyo:

“(6) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Afisa Mas-uli atawajibika kuhakikisha kwamba risiti zinatolewa kwa mapato yote yanayokusanywa na kwamba mapato yanapokewa, yanahifadhiwa na yanahesabiwa kwa ujumla wake.

(7) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, matumizi yoyote dhidi ya mapato yatahitaji idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali kama matumizi yaliyoingiwa na Serikali”.

Marekebisho ya kifungu cha 111.

**28.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 111, kwa kufuta aya (d) na kuzipa aya mpya (e), (f) na (g) kuwa aya (d), (e) na (f) kwa mpangilio.

Marekebisho ya kifungu cha 119.

**29.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 119, kwa kufuta nambari “3” ambayo inaonekana katika kifungu kidogo cha 2 baina ya maneno “kipindi cha” na “miezi” na kuweka badala yake neno “sita”.

Marekebisho ya kifungu cha 121.

**30.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 121, kwa kufuta nambari “118” ambayo inaonekana katika kifungu kidogo cha (4) na kuweka badala yake nambari “18”.

Kuongeza vifungu vipya vya 133A na 133B.

**31.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 133A na 133B mara baada ya kifungu cha 133 kama ifuatavyo:

“Muongozo wa utozaji kodi wa miradi ya maendeleo.

**133A.** (1) Bila ya kuathiri masharti ya sheria za kodi, Waziri anaweza kwa amri iliyotangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, kuweka Muongozo kutokana na misingi ya kimataifa ya kodi ili kurahisisha uamuzi wa ama kutoa au kutotoa misamaha ya kodi kwa Misaada Rasmi ya Miradi ya Maendeleo.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, muongozo utahusu tu utozaji wa kodi kwa miradi inayohusisha misaada ya kimaendeleo inayotolewa na serikali za kigeni na mashirika yake ya misaada na taasisi za kimataifa”.

“Kanuni kuidhinishwa na Waziri”.

**133B.** Bila ya kuathiri utozaji na misamaha iliyotolewa na Waziri husika katika masharti ya sheria husika katika kutoza ushuru wowote, ada au tozo au misamaha yake kama itakavyokuwa itahitaji kwanza idhini ya Waziri.

SEHEMU YA NANE
MAREKEBISHO YA SHERIA YA AJIRA NAM. 11 YA 2005

Kusomwa.

**32.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ajira Nam. 11 ya 2005, katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kuongeza kifungu kipya cha 38A.

**33.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 38A mara baada ya kifungu cha 38 kama ifuatavyo:

"Kushindwa kufanya upya kibali cha kazi".

38A. Muajiri ambaye ameshindwa kufanya upya kibali cha kazi au kuwasilisha taarifa ya usitishaji wa mkataba ndani ya siku kumi na nne kutoka tarehe ya kumaliza muda wa kibali au mkataba, kama itakavyokuwa, atalazimika kulipa Shilingi Laki Tano kwa kila siku thelathini ambazo amechelewa.

Kufuta na kubakiza kifungu cha 39.

**34.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 39, na kukiweka kifungu kipya cha 39 kama ifuatavyo:

"Msamaha au punguzo kwa ada ya vibali vya kazi".

39(1). Mwenye hisa binafsi ambaye uwekezaji wake una sifa ya kuwa uwekezaji mkakati au ambaye anamiliki zaidi ya asilimia ishirini ya uwekezaji ulioidhinishwa chini ya masharti ya Sheria ya Mamlaka Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar, atasamehewa malipo ya ada za kibali cha kazi.

(2) Muajiriwa mgeni ambaye ameajiriwa katika Taasisi ya Umma atasamehewa malipo ya ada za kibali cha kazi, ikiwa kuna makubaliano yaliyoeleza msamaha huo.

(3) Bila ya kujali masharti ya vifungu vidogo vya (1) na (2), Waziri anaweza, baada ya kushauriana kwa maandishi na Waziri anayehusika na Fedha, kutoa msamaha au pungunzo la malipo ya ada za kibali cha kazi, kama itakavyokuwa, iwapo itakuwa ni kwa maslahi ya umma.

## SEHEMU YA TISA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA UKUZAJI NA KULINDA VITEGA UCHUMI ZANZIBAR NAM. 14 YA 2018

Kusomwa.

**35.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mamlaka ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar Nam. 14 ya 2018, katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kuongeza kifungu kipya cha 31A.

**36.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 31A mara baada ya kifungu cha 31 kama ifuatavyo:

"Taarifa ya utekelezaji ya kila mwezi kuwasilishwa kwa Waziri".

31A. Wawekezaji Mkakati, kila wanapoingiza bidhaa, watafuata orodha iliyoidhinishwa kwa pamoja na ZIPA na Idara ya Forodha na watawasilisha kila mwezi ripoti ya utekelezaji kwa Waziri.

## SEHEMU YA KUMI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA NAM. 11 YA 2016

Kusomwa

**37.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Nam. 11 ya 2016, katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kuongeza kifungu kipya cha 73 A.

**38.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya 73A mara tu baada ya kifungu cha 73 kama ifuatavyo:

"Kuzibariki Taasisi za Serikali zenye uwezo".

73A. Bila ya kujali masharti ya Sheria hii, Baraza la Mapinduzi linaweza kuamua miradi yenye maslahi ya umma, usalama wa taifa na ya kimkakati inayofadhiliwa moja kwa moja na Serikali kubarikiwa kama mzabuni pekee kwa taasisi za Serikali zenye uwezo husika.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 18 Juni, 2020.

.............................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***